Faida za kozi kwenye jukwaa la mafunzo ya kielektroniki

Ukuzaji wa ujuzi kwa vitendo katika ulimwengu halisi ili kuboresha namna ya kufanya biashara, kuongeza ushindani, na kuangazia sera za biashara za kikanda.

Kuimarishwa kwa uwezo wa watu binafsi na biashara ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kusaidia moja kwa moja ushirikiano wa kikanda na ukuaji wa uchumi.

Kupokea cheti kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki ambacho kinaweza kuongeza uaminifu wa kitaaluma na kutoa fursa mpya za kazi katika nyanja zinazohusiana na biashara.

Wasiliana nasi

EAC Secretariat:
fbusingye@eachq.org
Mawasiliano ya Kozi:
jennifer.gache@gfa-group.de

Implemented by

atingi

KOZI ZA BIASHARA KATIKA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

Maarifa Kiganjani

Kuhusu Atingi

Atingi ni jukwaa la kidijitali la kujifunza linalolenga kutoa fursa za mafunzo yanayohusiana na mahitaji ya ujuzi muhimu nchini. Linalenga kuziba pengo la ujuzi muhimu katika ajira na elimu kwenye masoko yanayoibuka. Atingi ni jukwaa lililiopo katika lugha mbalimbali, linalozingatia sheria za GDPR kwa majukwaa ya elimu kwa njia ya kielektroniki, limeidhinishwa na Wizara ya Shirikisho la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo ya Ujerumani (BMZ) na kutengenezwa na GIZ.

Kozi kadhaa zimeandaliwa kupitia programu ya EAC-GIZ ya Biashara ya Bidhaa (TIG). Kozi hizo ni za bila malipo na zinaweza kufikiwa na wanafunzi kote katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwingineko, bila kujali mahali walipo na hivyo kukuza ushirikishwaji.

Walengwa wa Kozi

Kozi hizi zinawalenga: Wajasiriamali, Biashara Ndogo, Ndogo na za Kati (MSMEs), viongozi wa serikali na watunga sera, wataalamu wa biashara na wanafunzi, wasomi na watafiti, tanki ya fikra na yeyote anayevutiwa. Kozi hizi zinatoa maudhui ya kujifunza, nyenzo za ziada za kusoma, masomo kwa njia ya video, maswali ya mtihani, nafasi ya kubadilishana mawazo na cheti kilichothibitishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kozi hizi zimejitosheleza, zinatoa mafunzo kwa vitendo na zinaendana na uhitaji wa walengwa.

Kozi zinazotolewa

Jinsi ya kuwa Mwendeshaji Uchumi Aliyeidhinishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki.
Kozi hii itakusaidia kuzingatia viwango vya usalama vya kimataifa vya ugavi na kuidhinishwa na usimamizi wa forodha kusafirisha bidhaa wa kimataifa.

Viwango vilivyooanishwa vya Jumuiya ya Afrika Mashariki.
Kozi hii itakusaidia kutekeleza viwango vilivyooanishwa vya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mahitaji ya ubora na usalama katika matunda na mboga mboga na sekta za Ngozi.

Mbinu Bora za Usindikaji wa Ngozi na Utengenezaji wa Bidhaa za Ngozi.
Kozi hii itakuonyesha jinsi ya kutumia Mbinu Bora zenye viwango vya kimataifa za usindikaji wa ngozi.

Mwongozo Rahisi wa Biashara ya Mipaka.
Kozi hii imelengwa hasa kwa wakulima, wafanyabiashara, wachakataji wa mazao, na mtu yeyote anayetaka kuwa meneja wa biashara ambaye anataka kupanua biashara yake kwa kuuza bidhaa nje ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kuboresha Taratibu za Forodha za Jumuiya ya Afrika Mashariki.
Kozi hii inafafanua taratibu mpya za forodha za Jumuiya ya Afrika mashariki na fursa zinazotolewa kwa biashara za kikanda.

Skani QR Code kupata taarifa zaidi kuhusu atingi!

atingi.org @atingi_elearn atingi.org